**MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(MAHAKAMA JUMUISHI YA HUDUMA ZA MIRATHI NA NDOA)**

**INAYOKETI TEMEKE**

**SHAURI LA MIRATHI NA.06 2021**

**MARY MICHAEL MASENGE....................................MUOMBAJI 1**

**ROMAN JOVIN MASENGE......................................MUOMBAJI 2**

**POLYCALP JOVIN MASENGE..................................MUOMBAJI 3**

**ALLEX MICHAEL MASENGE...................................MUOMBAJI 4**

**ENIAD MICHAEL MASENGE....................................MUOMBAJI 5**

**LUDOVICK MICHAEL MASENGE.............................MUOMBAJI 6**

**PATRICK MICHAEL MASENGE................................MUOMBJI 7**

**CATHERINE MICHAEL MASENGE............................MUOMBAJI 8**

**DHIDI YA**

**KADINDA MICHAEL MASENGE**

**(Msimamizi wa mirathi ya marehemu**

**Michael Jovin Masenge)........................................MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI**

**Z.M.GORONYA, J.**

Mnamo tarehe 05/09/2022 waombaji waliwasilisha maombi chini ya kifungu 49(1)(b) cha Sheria ya Mirathi na usimamizi wa mali, Sura ya 352 RE 2019 na kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa mirathi, Tangazo la Serikali (TS.Na. 10/1963) wakiiomba mahakama itoe nafuu zifuatazo;

*i. Kwamba, mahakama hii tukufu kama itapendezwa imuondoe Kandida Michael Masenge, msimamizi wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge*

*ii. Amri yoyote Nyinginezo ambazo mahakama hii tukufu itaona ni stahiki kutolewa katika mazingira ya maombi haya.*

Kwa ridhaa ya wadaawa maombi haya yalisikilizwa kwa njia ya maandishi ambapo waombaji waliwakilishwa na Wakili Sakina Hussein Sinda, mjibu maombi aliwakilishwa na Wakili Mohamed Majaliwa.

Kabla ya kufanya mawasilisho yake juu ya maombi haya, Wakili Sinda aliieleza mahakama kuwa upande wa mjibu maombi haujawasilisha kiapo kinzani hivyo aliiomba mahakama ione kuwa mjibu maombi hajapinga maombi haya hivyo mahakama iridhie maombi kama yalivyowasilishwa na waleta maombi.

Kwaajili ya maombi, wakili Sinda alieleza kuwa hii si mara ya kwanza kwa Mjibu maombi kufungua shauri la mirathi kwa siri bila kuwashirikisha waombaji ambao pia ni wanufaika wa mirathi hii. Alieleza kuwa aliwahi fungua shauri la mirathi Namba 16/2017 katika mahakama ya Wilaya kinondoni ambapo aliteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge. Barua za usimamizi wake zilibatilishwa na mahakama Kuu, masjala ya Dares Salaam katika Shauri la Marejeo Namba 36/2020 tarehe 01/07/2021. Mjibu maombi hakuridhika na uamuzi huo hivyo aliwasilisha taarifa ya kukata rufaa.

Alieleza zaidi pamoja na taarifa hiyo ya rufaa, Mjibu maombi alifungua tena shauri hili la mirathi Na.06/2021 bila kuwashirikisha wajibu maombi na walipokuja kupata taarifa tayari alikuwa ameshateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi na ameshafanya hatua kadhaa za utekelezaji wa majukumu ya msimamizi wa mirathi. Alisisitiza kuwa mjibu maombi hakua sahihi kufungua shauri jipya la mirathi bila kuondoa taarifa yake ya kukata rufaa, ili kusisitiza hoja yake Wakili Kisinda alirejea shauri la **Moa General Trading Co.Ltd vs. Chrisak Farm na wengine 4**, Shauri la Ardhi Na.92/20209 (haijaripotiwa) ambapo ilielezwa kwamba jambo hili linainyima mamlaka mahakama kuu kusikiliza shauri hilo kwasababu jambo lililokatika mgogoro ndilo lililopelekea taarifa ya rufaa. Wakili Sinda alisisitiza kwamba, kwakuwa Mjibu maombi hakuondoa taarifa ya kukata rufaa, mahakama hii haikuwa na mamlaka ya kumteua kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge.

Zaidi ilielezwa kwamba, katika kikao cha kumteua msimamizi wa mirathi mjibu maombi alikaa yeye na watoto wake tu pasipo kuwashirikisha waleta maombi ambao ni mke na watoto wengine wa marehemu. Hivyo maombi yake yalikuwa batili kwasababu yalikosa ridhaa ya waombaji wambao pia niwanufaika wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge. Wakili Sinda, alieleza kwamba mjibu maombi katika orodha ya mali zilizoziweka ni pamoja na mali na waombaji na.2 na Nambari.3 ambao ni kaka wa marehemu. Alimalizia kwa kuiomba mahakama itengue uteuzi wa mjibu maombi uliotolewa na mahakama hii.

Kwa upande wa mjibu maombi, Wakili Majaliwa alieleza kuhusiana na suala la kutowasilisha kiapo kinzani kwa mujibu wa Kanuni ya 16 ya TS. Na. 10/1963, 107/1963 and 369 /1963 zitokanazo na Kifungu cha 9 cha Sura ya 352 ya mwaka 1963, ni hiyari ya mjibu maombi kutumia kiapo hususani kwa mashauri ya mirathi yaliyo chini ya kanuni za mirathi. Pia alieleza kuwa waombaji hawajaomba kiapo chao kuwa sehemu ya mawasilisho yao hivyo kiapo hicho hakipaswi kuzingatiwa na mahakama.

Wakili Majaliwa alieleza zaidi kuwa, maombi haya yameletwa chini ya Kifungu cha 49(1),(b) cha Sheria ya Mirathi na usimamizi wa mali Sura ya 352 lakini waombaji wameshindwa kuileza mahakama ni namna gani uteuzi wa Mjibu maombi ulipatikana kwa udanganyifu au kuificha mahakama jambo muhimu kwa mirathi ya marehemu. Hoja ya taarifa ya kukata rufaa iliyotolewa na mjibu maombi si miongoni mwa sababu zilizoainishwa na sheria zinazoweza kutengua uteuzi wa msimamizi wa mirathi. Kusisitiza maelezo yake alirejea shauri la **May Mgaya vs Sakimu Said(msimamizi wa mirathi ya Said Salehe) na Salehe Saidi (msimamizi wa mirathi ya Said Salehe)**, Rufaa ya Madai Nambari.264/2017 (haijaripotiwa). Wakili Majaliwa aliongeza kuwa Taarifa hiyo ya rufaa inayoelezewa na waombaji haipo tena baada ya kuondolewa mahakamani kama alivyothibitisha Mh. Naibu Msajili.

Zaidi, wakili Majaliwa alieleza kuwa waombaji 1,2, na 3 wote si warithi wa marehemu katika mirathi hii,wao ni ndugu wa marehemu wasio na haki ya kusimama na kulisemea shauri hili, wote wameshafunguliwa

mashauri dhidi yao na msimamiazi wa mirathi. Alimalizi a kwa kuiomba mahakama itupilie mbali maombi haya.

Katika hoja za majumuisho, wakili sinda alisisitiza mawasilisho yake ya awali na kuongeza kuwa kwa mjibu maombi kutowasilisha kiapo kinzani ni wazi kuwa hajapinga maombi haya, alirejea shauri la **Asha Ramadhani Mwambala vs. Mselemu Ramadhani**, Misc. Land Application No. 219/2018.

Baada ya kupitia mawasilisho ya pande zote mbili, kumbukumbu za shauri na sheria husika, maombi haya yatatautliwa kama ifuatavyo;

Kwa kuanzia na suala la mjibu maombi kutowasilisha kiapo kinzani, ni wazi kuwa maombi haya yameambatanishwa na kiapo cha waleta maombi, lakini mjibu maombi hakuwasilisha kiapo kinzani kupinga au kujibu maombi kwa kueleza kuwa ni hiyari ya kisheria kupinga maombi kwa kiapo au kutotumia kiapo, alirejea kanuni ya 10 ya TS.Na.10/1963 iliyoeleza kuwa; *"Where a respondent intends to use affidavits in opposition to an application, he shall deliver copies of such affidavits to the applicant not less than two days before the day appointed for the hearing."*.

Ni msimamo wa kisheria kwamba maelezo ya kiapo ni ushahidi na ni wazi kuwa ushahidi huo wa kwenye kiapo unapaswa kupingwa au kujibiwa kwa kiapo kinzani. Hii imeeelwa katika mashauri mbalimbali, mfano Mahakama ya Rufaa katika shauri la **Gilbert Zebedayo Mrema vs Mohamed Issa Makongoro** (Civil Application 369 of 2019) [2020] TZCA ilipokutana na mzaingira haya ilieleza:

> *"That evidence made under oath can only. be negated by affidavit in reply. As already pointed out, the respondent did not file any affidavit in reply to refute the applicants evidence given under oath. In the circumstances, we discard that submission coming from the bar".*

Mahakama ya rufani kwenye kesi hapo juu haikuzingatia mawasilisho ya mjibu maombi kwa kushindwa kuwasilisha kiapo kinzani. Nafuu pekee aliyonayo mjibu maombi ni kufanya mawasilisho yake kwenye masuala ya kisheria tu na sio ushahidi kama ilivyolezwa katika shauri la **Fatuma**

**Ally Mohamed Vs. Mohamed Salehe**, Misc. Land Application No. 365 of 2019,HC(haijaripotiwa). Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa mjibu maombi hajapinga ushahidi uliotolewa na mleta maombi kwa njia ya kiapo na mawasilisho yake yanayopinga ushaidi .

Pia hoja ya waleta maombi kutokuiomba mahakama kiapo chao kiwe sehemu ya mawasilisho yao, kama ambavyo imeelezwa na Wakili wa waleta maombi kutofanya hivyo sio kosa la msingi. Hii ni kutokana na kwamba kiapo hicho tayari ni sehemu ya kumbukumbu za shauri kwa upande wa waleta maombi na mahakama ni lazima itapitia nyaraka hiyo katika kufanya maamuzi yake, kama ilivyoelezwa pia katika mashauri mbalimbali ya mahakama mfano shauri la **Asha Ramadhani Mwambala vs. Mselemu Ramadhani**,*(supra)* na Shauri la **Roland Msumi & 3 others vs Amani Polyfibre Co. Ltd**, Rev. No. 102/2019. Hivyo hoja hiyo ya mjibu maombi haina mashiko.

Katika maombi haya waleta maombi wameiomba mahakama itengue uteuzi wa mjibu maombi kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge. Kwa mujibu wa Sheria, kifungu cha 49(1) Cha Sura ya 352 RE 2019, kimeainisha sababu ambazo mahakama inaweza kutengua hati ya usimamizi wa mirathi. Kimeeleza:

"Section 49 (1) *(a) that the proceedings to obtain the grant were defective in substance;*

***(b) that the grant was obtained fraudulently by making a false***
***suggestion, or by concealing from the court something material***
***to the case;***

*(c) that the grant was obtained by means of an untrue allegation of a fact essential in point of law to justify the grant, though such allegation was made in ignorance or inadvertently;*

*(d) that the grant has become useless and inoperative;*

*(e) that the person to whom the grant was made has wilfully and without reasonable cause omitted to exhibit an inventory or account in accordance with the provisions of Part XI or has exhibited under that Part an inventory or account which is untrue in a material respect."*

Waleta maombi wameleta maombi haya chini ya Kifungu cha 49(1) (b) kwamba**, uteuzi ulipatikana kwa njia ya udanganyifu kwa kutoa taarifa zisizo za kweli, au kwa kuificha mahakama jambo muhimu la mirathi husika.** Ieleweke wazi kwamba, mahakama itatengua au kubatilisha hati ya usimamizi pale tu itakapojiridhisha kuwa sababu zilizoainishwa katika fungu la 49(1) la Sura ya 352 RE 2019, kama lilivyoainishwa hapo juu. Hivyo ni jukumu la waleta maombi kuthibitisha sababu za kuomba kutengua hati ya usimamizi iliyotolewa kwa mjibu maombi. Katika kiapo chao waleta maombi wameeleza kuwa mirathi na 06/2022 ilifunguliwa wakati tayari mleta maombi amewasilisha taarifa ya rufaa tarehe 23/07/2022. Rufaa hiyo ilitokana na maamuzi katika shauri la Mapitio ya Madai Na.36/2020 ya Mahakama kuu, Masjala ya Dar es Salaam, ambapo tarehe 01/07/2021 ilitengua hati ya usimamizi ya mjibu maombi iliyotolewa katika Shauri la Mirathi na. 16/2017 iliyotolewa na mahakama ya Wilaya ya kinondoni. Kwamba bila kuondoa taarifa hiyo ya rufaa, Mjibu maombi kwa siri

alifungua Mirathi namba 6/2021 bila kutoa taarifa kwa waleta maombi ambao ni wanufaika wa mirathi hiyo.

Mahakama hii baada ya kupitia kumbukumbu za shauri hili imeona kuwa hakuna ubishani kwamba mjibu maombi alikwisha wasilisha taarifa ya rufaa dhidi ya marejeo ya madai na.36/2020 mnamo tarehe 23/07/2022, na kuwa alifungua shauri hili la mirathi kabla ya kuondoa taarifa hiyo katika mahakama ya Rufaa. Hili linathibitika na Amri ya mahakama ya rufaa ya kuondoa taarifa hiyo iliyotolewa tarehe 31/10/2022 wakati shauri hili lilifunguliwa tarehe 12/09/2021. Ni maoni ya mahakama hii kwa kitendo hiki cha mjibu maombi kufungua mirathi katika mahakama hii wakati akiwa hajaondoa taarifa hiyo ya rufaa ni matumizi mabaya ya mahakama na yenye nia ovu ya kuwanyima haki waleta maombi kwani, ni dhahiri kuwa walikuwa wakiendelea kusubiri muendelezo wa rufaa hiyo wakati yeye anaendelea na usikilizaji wa mirathi katika mahakama hii.

Pamoja na hayo, wajibu maombi wameeleza kuwa katika kikao cha kumteua Mjibu maombi kuwa msimamizi wa mirathi, hakuwashirikisha mke mdogo wa marehemu, muombaji nambari 1 na watoto wa marehemu waombaji nambari 4,5,6,7,na 8. Wao kama warithi wa marehemu hawakua wameridhia uteuzi huo hivyo maombi yaliyofunguliwa katika mirathi na.6/2021 yalikuwa batili kwakukosa ridhaa ya warithi (Consent of heirs) ambao ni waleta maombi na.1,4,5,6,7na 8 wanufaika wa mirathi na.6/2021. Mahakama baada ya kupitia kumbukumbu za shauri hili nimeona kuwa ni wazi kuwa shauri hili la mirathi lilifunguliwa bila hati za ridhaa (consent of heirs) za waleta maombi kama lilivyotakwa la kisheria chini ya kanuni ya 71(1)

ya Kanuni za Mirathi, TS.Na. 10/1963. Ni maoni ya makahama hii kuwa mjibu maombi alitoa taarifa za uongo juu ya kupendekezwa kwake kuwa msimamizi wa mirathi lakini pia kuificha mahakama kwa kufungua mirathi inayokosa baadhi ya hati za ridhaa za waleta maombi 1,4,5,6,7 na 8 ambao hata yeye anawatambua kuwa ni wanufaika wa mirathi hii. Mjibu maombi hakuweza hata kuweka kiapo cha wanufaika wasiotoa ridhaa kama inavyotakiwa katika kanuni ya 72 (1) ya TS.Na.10/1963. Pia kwa mujibu wa muhtasari uliowasilishwa mahakamani hapa waleta maombi 1,4,5,6,7 na 8 hawakuwa sehemu ya waliompendekeza mjibu maombi kuwa msimamizi wa mirathi.

Kutokana na hayo, mahakama imeona kuwa waleta maombi wameweza kuthibitisha kuwa mirathi hii Na.6/2021 ilifunguliwa kwa udanganyifu na mjibu maombi hivyo basi, natengua hati ya usimamizi wa mirathi ya marehemu Michael Jovin Masenge iliyotolewa kwa mjibu maombi na mahakama hii tarehe 09/11/2021. Wadaawa wanahaki ya kufungua shauri la mirathi upya katika mahakama stahiki. Imeamriwa hivyo.

Z.M. Goronya

**Judge**

26/05/2023

Uamuzi huu umesomwa leo mbele ya Sakina Sinda, wakili wa waleta maombi na Mohamed Majaliwa, wakili wa Mjibu maombi.

Z.M. Goronya

**Judge**

26/05/2023